



## **AZIMIO NA. 7/2014**

### **AZIMIO LA BUNGE LA ITIFAKI YA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI KUHUSU USHIRIKIANO KATIKA MASUALA YA KIULINZI (*THE EAST AFRICAN COMMUNITY PROTOCOL ON COOPERATION IN DEFENCE AFFAIRS*)**

**KWA KUWA**, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi mwanachama wa Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu Ushirikiano katika Masuala ya Kiulinzi (*The East African Community Protocol in Defence Affairs*);

**NA KWA KUWA**, kabla ya kukubaliwa kuwepo kwa Itifaki hii, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zilikuwa na makubaliano ya kushirikiana katika masuala ya Nyanja mbalimbali za kiulinzi yanayojulikana kama *"Memorandum of Understanding on Cooperation in Defence"*;

**NA KWA KUWA**, kutokana na kupanuka kwa masuala nyeti ya kiulinzi ambayo yalishindwa kushughulikiwa chini ya makubaliano hayo, Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Mkutano wao wa 10 wa dharura uliofanyika Arusha tarehe 28 Aprili, 2012, waliridhia kupandisha hadhi makubaliano hayo kuwa Itifaki ya Ushirikiano katika Masuala ya Kiulinzi;

**NA KWA KUWA,** kuna umuhimu wa kushirikiana katika masuala yote ya ulinzi na kufanya kazi pamoja na Jumuiya za Kikanda na Kimataifa ili kuimarisha amani, usalama na utatuzi wa migogoro na pia kushirikiana katika mafunzo ya kijeshi na operesheni za pamoja;

**NA KWA KUWA,** kwa kujiunga na Itifaki hii, Tanzania itafaidika kutokana na kuimarika kwa amani, ulinzi na utengamano miongoni mwa nchi wanachama na kuwepo kwa mazingira ya amani kwa ajili ya maendeleo endelevu, kuwepo kwa mfumo wa kushughulikia migogoro, kuzuia au kukabiliana na ugaidi wa kimataifa katika nyanja zote;

**NA KWA KUWA,** pamoja na kutoa fursa kwa nchi jirani kufahamu shughuli zetu za ulinzi, Serikali itachukua tahadhari kudhibiti mbinu zetu za ulinzi ili zisijulikane kwa lengo la kuimarisha usalama wa Nchi yetu;

**HIVYO BASI,** Bunge hili katika Mkutano wake wa Kumi na Sita na Kumi na Saba na kwa Mujibu wa Ibara ya 63 (3) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977, linaazimia kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu ushirikiano katika Masuala ya Kiulinzi yaani (*The East African Community Protocol on Cooperation in Defence Affairs*).

Limepitishwa na Bunge leo tarehe 24 Novemba, 2014.

Dkt. T. D. Kashililah  
**KATIBU WA BUNGE**